

TAASISI YA ELIMU TANZANIA (TET)
Tanzania Institute of Education (TIE)

Telephone: +255-22-2773005

Fax: +255-22-2774420

Mail: director.general@tie.go.tz

Website: <http://www.tie.go.tz>



P. O. Box 35094,

Dar es Salaam,

TANZANIA.

23/4/2018

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UANDISHI, UCHAPAJI NA USAMBAZAJI
WA VITABU VYA KIADA VYA DARASA LA I-IV KWA MWAKA 2018**

Hii ni kuufahamisha umma wa Tanzania kuwa, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imekamilisha uandishi wa vitabu aina 24 kwa Darasa la I-IV na vitabu aina saba vya Kiongozi cha Mwalimu kwa Darasa la Nne. Vitabu hivyo viko katika hatua ya uchapaji na usambazaji shuleni na vimeshasambazwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Tanga, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Mwanza, Pwani, Morogoro, Lindi na Iringa. Kazi ya usambazaji inaendelea kukamilishwa katika mikoa iliyobaki. Vitabu vya Kiongozi cha Mwalimu darasa la nne vitasambazwa sambamba na kitabu cha Mwanafunzi. Orodha ya vitabu kulingana na darasa ni kama ifuatavyo:

Vitabu vya Darasa la I

1. Kusoma Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza Kitabu cha Kwanza
2. Kusoma Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza Kitabu cha Pili
3. Kuandika Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza
4. Kuhesabu Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza
5. Afya na Mazingira Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza
6. Michezo na Sanaa Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza

Vitabu vya Darasa la II

1. Kusoma Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili
2. Kuandika Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili
3. Kuhesabu Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili
4. Afya na Mazingira Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili
5. Michezo na Sanaa Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili

Vitabu vya Darasa la III

1. Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu
2. Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu
3. Sayansi na Teknolojia Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu
4. Hisabati Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu
5. Maarifa ya Jamii Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu
6. English Standard Three Pupils' Book

Vitabu vya Darasa la IV

1. Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne **pamoja na** Kiswahili Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Nne
2. Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne **pamoja na** Uraia na Maadili Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Nne
3. Sayansi na Teknolojia Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne **pamoja na** Sayansi na Teknolojia Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Nne.
4. Hisabati Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne **pamoja na** Hisabati Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Nne
5. Maarifa ya Jamii Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Nne **pamoja na** Maarifa ya Jamii Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Nne
6. English Standard Four Pupils' Book and English Standard Four Teacher's Guide
7. Bonjour Les Amis! Methode de Francais Livre de l'eleve 2- Bonjour Les Amis Methode de Francais Livre du Professeur 2 Enseignement de Base: Cycle 1 Quatrieme Annee

Dkt. Aneth A. Komba
MKURUGENZI MKUU
Taasisi ya Elimu Tanzania.